Jumatano Januari 7, 2026 Pg 3 Uhuru

# Mabasi ya mwendokasi yafike Mbezi kuanzia leo- Shemdoe

**Na ATHNATH MKIRAMWENI**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Profesa Riziki Shemdoe, ameuagiza Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (UDART) kuanzia leo mabasi ya mwendokasi yafike Mbezi hadi Hospitali ya Muhimbili-Mloganzila.

Alisema lengo la agizo hilo ni kuondoa kero ya usafiri inayowakabili wananchi, hususan wagonjwa na ndugu zao.

Profesa Shemdoe alitoa maagizo hayo jana, jijini Dar es Salaam wakati akikagua fedha zilizotolewa na serikali zaidi ya sh. bilioni 1.2 kwa lengo la kununua vipuri vya ukarabati wa mabasi ya mwendokasi yaliyoharibika.

Alieleza wananchi wamekuwa wakilazimika kushuka Kimara au Mbezi na kutumia usafiri mwingine kufika Mloganzila, jambo linalosababisha ucheleweshaji na msongamano wa abiria.

Waziri huyo aliagiza UDART kuanzisha na kuboresha vituo vya kukatia tiketi katika njia husika, huduma iwe rahisi, salama na yenye mpangilio.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imetoa sh. bilioni 1.2 za ununuzi wa vipuri vya mabasi 30 yaliyoharibika kuyarejesha barabarani. Hadi hivi sasa mabasi 17 yameshakarabatiwa na muda wowote yataanza kutoa huduma.

Mbali na mabasi yaliyofufuliwa, serikali imetoa sh. bilioni 20 kununua mengine mapya 99, ambapo 49 tayari yamewasili bandarini.

"Mabasi mapya yataratibiwa kuanza kazi haraka kuongeza idadi ya mabasi barabarani. Huduma mpya itapanuliwa hadi njia za Kimara na Gongolamboto kufanikisha usafiri wa uhakika kwa maeneo yenye msongamano wa abiria,"alisema waziri huyo.

Kuhusu gharama za uhifadhi bandarini, Waziri Shemdoe aliagiza mabasi yote yatolewe haraka, taratibu za malipo ya kodi na uhakiki wa mabasi zitatimizwa kwa ushirikiano na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Profesa Shemdoe alifafanua hakuna mgongano wowote wa ulipaji kodi, kwani mabasi yote mali ya umma na fedha za ununuzi zimefadhiliwa kupitia hazina ya serikali, huku taratibu za malipo zikishughulikiwa kwa uwazi na uangalizi wa karibu.

**MADEREVA WAMENOLEWA**

Kuhusu changamoto za awali, Waziri Shemdoe alisema madereva wa mabasi wamepewa mafunzo maalumu kuhakikisha uendeshaji wa kitaalamu na kupunguza uharibifu wa mara kwa mara.

Alisema maboresho yote yanalenga kurahisisha usafiri wa umma, kupunguza adha kwa wakazi wa Dar es Salaam na kurejesha imani ya wananchi kwa huduma ya mabasi yaendayo haraka.

Mkurugenzi Mkuu wa UDART, Pius Ng'ingo aliahidi kutekeleza maagizo hayo mara moja huku akiwaomba wananchi kutumia vizuri usafiri huo na kuacha tabia ya kuharibu miundombinu ya usafiri.

CamScanner

HabariLeo Jumatano
Januari 7, 2026



# Serikali yaagiza mwendokasi kufika Mloganzila kuanzia leo

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imeagiza Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (UDART) kuhakikisha usafiri wa mwendokasi unafika Mbezi hadi Hospitali ya Mloganzila kuanzia leo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Profesa Riziki Shemdoe alitoa agizo hilo jana akikagua maendeleo ya ukarabati wa mabasi ya mwendokasi yaliyoharibika.

Serikali imetoa zaidi ya Sh bilioni 1.2 kwa ajili ya ununuzi wa vipuri vya ukarabati wa mabasi chakavu 10 ya mwendokasi ili kuondoa kero ya usafiri iliyopo na mpaka sasa tayari mabasi 17 yamesharekebishwa.

"Hapa tunafika Kimara Mwisho lakini tuna maeneo yanahitaji huduma sana eneo la Mloganzila hospitali… nikupe maelekezo kuanzia kesho (leo) hakikisha tunapata mabasi yanayofika Mloganzila hospitali," aliagiza.

Aliongeza: "Watu wanapata shida; wana wagonjwa kule, wagonjwa pia wanapata shida kufika kule ni vyema hili tukalichukulia kwa umuhimu wake."

Sambamba na agizo hilo, Profesa Shemdoe aliitaka UDART kuhakikisha wanatengeneza vituo vya kukatia tiketi vya muda vitakavyowawezesha wananchi wanaotumia usafiri huo kupata urahisi wa kukata tiketi.

Aidha, Profesa Shemdoe alisema serikali imetoa Sh bilioni 20 kwa ajili ya ununuzi wa mabasi 99 na tayari mabasi 49 yameshaingia bandarini na kuwataka wakala hao kuhakikisha wanayatoa mabasi hayo bandarini na kuyaweka sehemu ili kusaidia kupunguza gharama za kodi yakiendelea kuwepo hapo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu UDART, Pius Ng'ingo alisema utekelezaji wa agizo hilo utafanyiwa kazi na kuwaomba wananchi kutumia vizuri usafiri huo na kuacha tabia ya kuharibu miundombinu ya usafiri.

Alisema tayari imetoa mafunzo kwa madereva watakaoendesha magari hayo ili kupunguza changamoto ya magari kuharibika kutokana na madereva kukosa uzoefu.

CamScanner